# Utekelezaji wa Maazimio ya Mkutano wa sita wa wadau wa kahawa 28-29, Mei, 2015.

| NO. | AZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| 1. | Halmashauri ziwasilishe taarifa ya kiasi cha fedha walizopata kutokana na ushuru wa Kahawa na kiasi kilichotumika katika kuendeleza zao la Kahawa. | Halmashauri za wilaya, TCB | Taarifa imembatanishwa |
| 2. | Halmashauri zitumie asilimia 20 ya fedha za mapato yatokanayo na ushuru wa Kahawa katika kuendeleza zao la Kahawa hususani mafunzo kwa maafisa ugani wa Kahawa na uzalishaji miche. | Halmashauri za wilaya | Taarifa imeambatanishwa |
| 3. | TaCRI ishirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Tarime kufuatilia upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha utafiti wa Kahawa Wilayani Tarime. | Halmashauri ya Tarime, TaCRI, TCB | Bodi ya TaCRI ilifuatilia na kufanya kikao chake cha 41 tarehe 12- 13 Novemba 2015 Sirari Tarime na kuonana na Mkurugenzi wa H/Wilaya Tarime ambaye aliahidi kufuatilia upatikanaji wa Ardhi. |
| 4. | Serikali itimize ahadi yake ya mwaka 2012 ulipoanzishwa Mfuko wa Maendeleo ya Kahawa (TCDTF) ya kuchangia fedha kiasi cha Shilingi bilioni mbili. | Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, Mfuko (TCDF), | Taarifa ya utekelezaji wa azimio hili itatolewa kwenye taarifa ya TCDF. |
| 5. | Waingizaji wa vipando nchini wafuate utaratibu wa uingizaji wa miche/mbegu za zao la Kahawa ili kudhibiti ubora wa kahawa nchini. | Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, Halmashauri za wilaya na waingizaji | Halmashauri ya Wilaya ya Ileje ambako ndiko kulibainika tatizo la kingizwa kwa vipando kutoka nje ya nchi ilichukua hatua zifuatazo :<br>i. Iliandika barua kutaarifu taasisi ya utafiti wa Kahawa TaCRI – Mbimba na TCB – Kanda.<br>ii. Wataalamu kutoka TaCRI (HQ) Lyamungu na TaCRI – Mbimba walifika tarehe **08/04/2013** kufanya ukaguzi wa aina ya miche ya kahawa kutoka nchi ya Malawi ambayo ilikuwa imepandikizwa na baadhi ya wakulima.<br>iii. TaCRI waliwezesha upatikanaji wa miche ya jamii mpya za Kahawa aina ya *Compact* ambazo zilipandikizwa katika Ploti mbili kwa ajili mafunzo katika Kijiji cha **Kafule** na Kijiji cha **Kalembo**<br>iv. Matokeo mazuri yaliyoonekana katika plot hizi za mfano yamesaidia wakulima kuacha ile tabia ya kuamini kuwa miche kutoka nje ya nchi ndio bora kuliko iliyopo nchini. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6. | TaCRI iongezewe uwezo wa kifedha ili iweze kuendelea kufanya utafiti, kutoa mafunzo ya ugani na huduma za kitaalamu kwenye zao la kahawa. Vile vile Mfuko wa Maendeleo ya Kahawa (TCDF) uongezewe uwezo katika kutekeleza majukumu yake.<br>Wadau wa kahawa wanapendekeza kuwa kiwango cha uchangiaji kiwe kama ifuatavyo:<br>a) TACRI kutoka 0.75% hadi 1.0%.<br>b) TCDF kutoka 0.2 hadi 1.0% | TaCRI, TCDF, Wadau | Azimio hili halikutekelezwa kwa sababu<br>1. Wadau wa kahawa hawakusaini na kubadili randama ya makubaliano (MOU) ili kuyapa mabadiliko haya ya viwango vya uchangiaji kuwa ya kisheria.<br>2. Utekelezaji wake unahusu mamlaka zaidi ya moja<br><br>Azimio hili linarudishwa kwa wadau kuamuliwa upya. |
| 7. | TaCRI iandae na kupendekeza mpango mkakati wa kuimarisha ugani na pamoja na mfumo thabiti wa uzalishaji miche. | TaCRI | Bodi ya TaCRI imetafakari na kuamua kuendelea kushiriki katika kazi ya kuchangia uzalishaji miche na kuimarisha ugani ikilenga zaidi kuwajengea wadau uwezo, kupanua wigo wa uzalishaji miche pamoja na utoaji wa huduma za ugani. |
| 8. | Bodi ya kahawa itoe elimu juu ya bei elekezi na kutoa tathmini ya utekelezaji wake. | TCB | Bodi ya kahawa imeendelea kutoa elimu juu ya bei elekezi ya kahawa kupitia njia mbalimbali kama redio, ofisi za bodi za kanda, ziara za kuwafikia wakulima, Mikutano mbalimbali ya wadau wa kahawa. |
| 9. | Kodi na michango/makato anayokatwa mkulima zirekebishwe ili kumpunguzia mkulima mzigo. | Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, TAMISEMI | Serikali imekwisha kusanya taarifa za kodi, makato na michango yote inayotozwa katika sekta ya kahawa na taarifa hizo zimekwisha chambuliwa na kuwasilishwa kwenye ngazi mbalimbali za maamuzi kwa ajili ya mapendekezo ya marekebisho ya kodi na makato mbalimbali kwenye sekta ya kahawa na kilimo kwa ujumla. |
| 10. | Ushiriki wa wanawake kiuchumi kwenye sekta ya kahawa uongezeke na inapendekezwa isipungue | TAWOCA, TCB, Wadau | Taarifa ya jitihada zinazofanywa na wadau kuongeza ushiriki wa wanawake sekta ya kahawa itawasilishwa kwenye taarifa ya TAWOCA |
| 11. | Wawekezaji wakubwa wa kahawa nao wapewe fursa ya kushiriki kwenye mkutano mkuu wa kahawa | TCB, Wadau | Washiriki wa mkutano mkuu wa wadau wa kahawa wameainishwa kwenye kanuni za kahawa 2013. Wawakilishi wa makundi yote ya wadau kama yaliyoainishwa kwenye kanuni wamealikwa na ni wajumbe kwenye mkutano huu. |
| 12. | TaCRI iimarishe mfumo wa utoaji taarifa za tafiti mbalimbali wanazozifanya ili ziwafikie wadau katika maeneo yanayohusika | TACRI | TaCRI imeendelea kuimarisha mfumo wa utoaji taarifa za kitafiti kwa kutembelea wakulima, wadau wengine, kutoa mafunzo vijijini na kwenye vituo vyake, kuandaa na kushiriki katika maonyesho ya kilimo, kusambaza vipeperushi na kutoa taarifa kwenye vyombo vya habari (Television, Redio na Magazeti) |
| 13. | Wadau wameazimia kwamba juhudi zifanyike kuwaelimisha wakulima wa Kagera kutumia mbolea ili kuboresha zao la kahawa | TCB, TCDF, Wadau Kagera | Juhudi mbalimbali zinafanyika kuwaelimisha wakulima wa Kagera umuhimu wa matumizi ya mbolea kwenye kilimo cha kahawa. Wadau mbalimbali Mf. TaCRI, Mradi wa CPT, H/Wilaya, Shirika la Kaderes wanajihusisha na utoaji wa mafunzo kwa wakulima ikiwa ni pamoja na umuhimu wa matumizi ya mbolea. |